

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Simu: 026-2782169,
Fax No. 026-2782178
e-mail rpc_njombe@tpf.go.tz



Ofisi ya,
Kamanda wa Polisi,
Mkoa wa Njombe,
S. L. P 08,
NJOMBE.

12/02/2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu waandishi wa habari,

Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe linaendelea na jukumu lake la kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao hadi kufikia tarehe 12/02/2022 hali ni shwari na salama licha kuwepo na mafanikio ya kukamatwa kwa mtuhumiwa wa kesi ya mauaji mkoani Njombe.

Ndugu waandishi wa habari,

Tarehe 08.02.2022 huko Mtaa wa Bwawani Kata ya Mjimwema Tarafa ya Makambako wilaya na Mkoa wa Njombe, **Paschal Otieno Makhoha** miaka 50, Mkristo Padri wa Parokia ya Makambako mkazi wa mtaa wa Bwawani aligundua kuuawa kwa **Nickson Elias Myamba**, miaka 46 Mbena Mkristo mkazi wa mtaa wa Kahawa Makambako baada ya kupigwa na kitu kizito kichwani upande wa kulia na mtuhumiwa **Daniel Philipo Mwelango** kisha mwili wake kukatwa na kutenganishwa vipande viwili na kufungwa ndani ya mfuko wa salphate na ndani ya box na kisha kufungiwa ndani ya duka la Kanisa la Roman Catholic Makambako, marehemu Nickson Elias Myamba alikuwa ni Katibu wa Kanisa la Roman Catholic Parokia ya Makambako ambapo tarehe 07.02.2022 majira ya saa 11:00hrs marehemu alitwa na mtuhumiwa Daniel Philipo Mwelango kwenda kwenye duka la kanisa kwa ajili ya kukabidhiana fedha baada ya kuwepo ubadhilifu wa fedha toka marehemu aingie dukani hapo akiwa na mtuhumiwa hakuonekana hadi mwili wake ulipokutwa ndani ya duka hilo ukiwa umetenganishwa kiwiliwili.

Ndugu waandishi wa habari,

Eneo la tukio kumekutwa mlango wa duka hilo ukiwa umefungwa na kufuri, mavazi ya kwaya ya kanisani yakiwa na matone ya damu, mifuko ya sulphate ikiwa na matone ya damu, shati lenye matone ya damu.

Kiini cha tukio ni tamaa ya kipato na kuficha ubadhilifu wa fedha uliofanywa na mtuhumiwa, watuhumiwa kumi na tatu (13) wamekamatwa kuhusiana na tukio hilo. Jeshi la Polisi lilifanikiwa kwenda kwenye tukio na kufanikiwa kukuta vitu vifuatavyo;

1. Mifuko ya sulphet 03 na mifuko na nailon 4.
2. Box 01.
3. Matambaa ya kudekia.
4. Majoho yaliyotapakaa damu.
5. Suruali yenye damu.
6. Pesa 785500/= sarafu na noti.

Ndugu waandishi wa habari,

Mtuhumiwa Daniel Mwelango miaka 42, Katekista baada ya tukio alikimbilia Dar es salaam lakini baadaye alikamatiwa kijiji cha Doma wilaya ya Mvemero mkoa wa Morogoro akitokea Dar es salaam tarehe 10/02/2022 majira saa 21:30hrs akiwa na vielelezo kama ifuatavyo;

1. Simu 01 ya marehemu.
2. Alikutwa tsh 120000/=.
3. Laini ya tigo mpya.
4. Funguo za dukani.
5. Begi la nguo mbalimbali la mtuhumiwa.

Aidha, mtuhumiwa baada ya kuhojiwa pia alionyesha vielelezo mbalimbali kama ifuatavyo;

1. Kipande cha chuma kilichotumika kumpiga marehemu.
2. Ndoo nyeupe iliyotumika kudekia damu.
3. Panga lenye damu lilokutwa ndani ya shimo la choo cha shule ya msingi makambako.
4. Funguo za duka zilizotambuliwa.

Wito

Kwanza: Wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoa wa Njombe katika kuhakikisha Mkoa wetu unaendelea kuwa salama wakati wote.

Pili: Wananchi waendeleo kutoa taarifa za waalifu na uhalifu ili wale wote wanaojihusisha na uhalifu wakamatwe na kuchukuliwa hatua stahiki

Tatu: Wananchi waachane na imani potofu ambazo zinaacha taharuki kwa jamii.

Aksanteni kwa kunisikiliza

Imetolewa na:

Hamis S. Issah - ACP

KAMANDA WA POLISI MKOA WA NJOMBE